**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
MWONGOZO WA KUSAHISHA

**1. UFAHAMU**

1. - Kuelimisha akina mama wazinduke ili waweze kujitegemea kiuchumi
   - Kuhamasisha maendeleo ya wanawake. (alama2)
2. - Waliunga mkono sera nzuri ya kusaidia wanawake (alama 2)
3. - Wao waliwanyanyasa wanawake kwa sababu ya ubabadume hasa katika kuwanyima wanawake fursa ya kujikimu kimaisha . (alama 2)
4. - Wao wamepata mikopo na kuanzisha biashara zao wenyewe (alama 1)
   - Wao wananunua ardhi yao sasa.
5. - Imani potovu eti wanaume ndio wanaostahili kuleta riziki (alama1)
   - Kutokopa fedha za kuanzisha biashara zao wenyewe (alama1)
   - Kuamini kwamba utajiri ni hifadhi ya wanaume (alama 1)
6. (i) kuwaza /kufikiria kwa makini (alama 1)
   (ii) kuwaondoa katika umaskini ulokithiri (alama1)
   (iii) pato la kusaidia mahitaji ya kimsingi ya kila siku (alama 10)

**SEHEMU YA B - UFUPISHO**


(a)

- Urafiki huleta mapatano
- Rafiki mwema hajali hali , urafiki au umaskini /au kuwa na cheo.
- Humuunga mkonowe katika raha na shida
- Huweza kutoa kila kitu na kuingia kumwokoa rafiki yake
- Rafiki adili ni bora kuliko ndugu wa tumbo moja
- Urafiki huo una Baraka na neema.
- Urafiki hudumu_hadi kutenganishwa na kifo ***(7×1=7 )***

(b)

- Urafiki ni lazima katika maisha
- Ni bora kuwa na marafiki wengi japo kuna hatari ya kupata waongo
- Ni bora tuwachunge marafiki na kujitenga na waovu
- Tushike fitina za watu bali tunahakikisha uovu wa mtu kwanza
- Kutambua rafiki mwovu ni rahisi lakini si haki kumwacha aangamie katika uovu bali tumwonye

***(5×1=alama 5)***





***(i) Mtahiniwa akifanyua makosa ya sarufi aondolewe ½ maki hadi makosa 6 baada ya kutuzwa.***
***(ii) mtahiniwa akifanya makosa ya tahjia aondolewe ½ maki hadi makosa 6 baada ya kutuzwa.***
***(6× ½ =alama 3) (inahusu ufahamu na muhtasari)***

**(c) MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

1. Kutungia neno wa'lakini sentensi.
   Wa'lakini ni nomino yenye maana ya dosari/kasoro/ila
   Mfano Gari langu lina walakini ***(1×1=1)***
2. Sifa tatu za /th/
   (i) Ni konsonanti
   (ii) Ni sauti sighuna /hafifu
   ***(iii)*** Hutamkiwa kwenye meno. ***(3×1=3)***
3. Mzizi wa neno 'machweo'
   _chw_ ***(2×1=2)***
4. Ukubwa:
   Jike la zee hili hupenda matoto sana
5. Kuyakinisha :
   Otoyo akija mwalimu atasahihisha kazi. ***(1×2=2)***
6. Matumizi mawili ya 'po'
   (i) 'po' mahali
   Mfano : Anapolala pana uchafu.
   (ii) po wakati
   Mfano: Alalapo hukoroma.
7. Matumizi mawili ya koloni kwa kutoa mfano wa sentensi
   (i) kutanguliza orodha ya maneno
   Mfano: Kuna njia mbili tu za kufaulu maishani:bidii na nidhamu.
   (ii) kutanguliza maelezo fulani
   Mfano:
   Mama alianza: "mimi sitaki Kuwa ninarudia jambo moja moja Kila siku na hakuna yule anayotaka Kunisikiliza" ***(2×1=2)***
8. Kuunda nomino mbili kutokana na kitenzi kinai
   (i) ukinaifu
   (ii) mkinaifu (wakinaifu) ***(2×1=2)***
9. Kutunga sentensi kudhihirisha ngeli ya ku -
   Mfano : ***Umoja*** - <u>ku</u>cheza huko hakufai
   ***Wingi*** - kucheza huko hakufai ***(1×1=1)***
10. Kubainisha yambwa.
    Askofu - yambwa tendewa
    Barua - yambwa tendwa ***(2×1=2)***
11. Kubainisha virai:
    <u>Chake chote</u> kilivunjika <u>vibaya sana</u>
    Kirai nomino kirai kielezi ***(2×1=2)***
12. Kuchanganua kwa matawi
    Ibada ya wafu iliyofanyika jana usiku ilisababisha kilio kingi.

Sentensi changamano




***(8 x ½ = 4)***

13. kutunga sentensi moja kutofautisha thibiti na dhabiti.
    Thibiti kuwa ya ukweli
    Dhibiti tunza,weka chini ya mamlaka
    Mfano :Askari alithibitisha kuwa gari hilo lilikuwa na kidhibiti mwendo. ***(2×1=2)***
14. kuandika katika usemi wa taarifa .
    Koinange alishangaa kwa jinsi ambavyo mawimbi ya tsunami yaliangamiza biashara nyingi sana.
    ***(2×1=2)***
15. (i) mofimu ni kipashio kidogo zaidi katika lugha
    (ii) Aina
    Mofimu huru:Mofimu ambazo huweza kujisimamia na kuwa na maana kamili bila kutegemea mofimu nyingine mifano kuku,mama ***(1×1=1)***
    Mofimu tegemezi:ni viungo vya maneno yenye maana Fulani lakini haviwezi kujitegemea vikiwa peke yake. ***(1×1=1)***
16. Hali ya mazoea kwa kutumia kirejeshi mwafaka.
    Mtoto alaye lishe bora ndiye akuaye vyema. ***(1×2 =2)***
    Tanbihi :mwanafunzi atumie ‘o’ rejeshi tamati hili kuzua dhana ya mazoea.
17. Kinyume:
    Wanaskauti wengi walipiga kambi jana asubuhi. ***(1×2=2)***
18. Kutunga kitenzi kishirikishi kipungufu (t) sentensi
    Vitenzi ‘vishirikishi vipungufu haviwezi kuambishwa viambishi vyovyote
    Mifano :ni,ki,li,yu,zi n.k
    ***Mfano***
    (i) mimi <u>ni </u>mzee
    t
    **(ii)** Daudi <u>yu</u> ukumbini
    T ***(1×1=1)***
19. Kutungia mzizi-enye sentensi kama kiwakilishi.

Mfano:

Mwenye macho haambiwi tazama
W *(1×2=2)*

20. Matumizi ya _ndi_
kurejelea nomino *(1×1=1)*
Adhabu.

(i) mtahiniwa akifanya makosa ya sarufi aondolewe ½ maki hadi makosa 6 baada ya kutuzwa.
***6×1/2=3***

(ii) mtahiniwa akifanya makosa ya tahajia aondolewa1/2 maki hadi makosa 6 baada ya kutuzwa
***6×1/2=alama 3***

**ISIMU JAMII** **(alama10)**

1. Ukosefu wa ufasaha wa lugha/elimu
2. kufahamu lugha zaidi ya moja
3. kuficha siri
4. kujitambulisha na kundi fulani hasa vijana
5. Kurithishwa na wazazi (vijana)
6. Haina (sheng)masharti (lugha legevu)
7. Uwezo mkubwa wa kukabilianana mazingira (ubunifu wa hali ya juu)

***(zozote 5×2=alama 10)***